**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA CHATO**

**Namba za simu**
**Mkuu wa shule** *+255 719 801 205*
**Makamu Mkuu wa Shule** +255 749 734 508

**SHULE SEKONDARI BWONGERA,**
**S.L.P 137,**
**CHATO - GEITA**

---

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi: …………………………………………

S.L.P……..

YAH: **MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BWONGERA HALMASHAURI YA WILAYA CHATO MKOA WA GEITA**

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **………….** tahasusi ya EGM/ HGE. Nakupongeza na karibu sana Bwongera sekondari.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ………………**.** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **…………. .**Mwisho wa kuripoti ni tarehe **……………….**. Ukifika shuleni utapokelewa na makamu mkuu wa shule na kusajiliwa katika daftari maalumu la kusajilia wanafunzi (Student Admission Register Book).

**<u>MAHALI SHULE ILIPO</u>**

Shule ya Sekondari Bwongera, ipo katika Wialaya ya Chato katika Mkoa wa Geita Kata ya Bwongera, kijiji cha katete, kitongoji cha Mkuyuni. Kuna umbali wa km 13 kutoka stendi ya mabasi mganza mpaka shule ilipo.

**<u>NAMNA YA KUSAFIRI KUFIKA SHULE YA SEKONDARI BWONGERA.</u>**

Kwa wanaopitia au kuanzia safari zao Mwanza wanapanda mabasi yaendayo Bukoba au yanayoishia Muganza na kuteremka Chato.

1. Kwa wanaotoka Dar es Salaam Morogoro, Dodoma au Singida wanaweza kupanda mabasi yaendayo Mwanza kisha apande mabasi ya Mwanza-Chato au anaweza kupitia Mwanza na kupanda mabasi yaendayo Bukoba na kutelemka kituo cha mabasi Mganza.
2. Kwa wanaotoka karagwe kupitia Bukoba, watapanda mabasi yaendayo Mwanza na watashukia kituo cha mabasi Mganza.
3. Kwa wanaotoka Kigoma, watapanda mabasi yaendayo Mwanza kupitia Runzewe wakifika Bwanga watashuka na kupanda magari yaendayo Chato- Muganza, na kushukia kituo cha mabasi Mganza.
4. Kwa wanaotoka Ngara kupitia Biharamulo, wakifika Biharamulo watapanda magari madogo yaendayo Chato-Mganza na kushukia kituo cha mganza.

   **NB** Wote hawa wakifika Chato-mganza kituo cha mabasi watateremka na Wakiulizia mtu yeyote atawaonyesha shule ilipo. Usafiri ni wa pikipiki au bajaji watakuleta shule ilipo.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 Sare za Shule

1. Shati nyeupe (2) mbili za mikono mirefu
2. Suruali (2) mbili za rangi ya bluu bahari pamoja na tai zake.
3. Suruali mbili (2) za rangi nyeusi kwa ajili ya shughuli za jioni
4. Soksi nyeusi, viatu vyeusi na mkanda wa ngozi mweusi
5. Sweta moja la bluu bahari, t-shirt moja ya Karoti ya kora 6 (Yenye nembo ya shule).
6. Track suti rangi ya blue
7. Vifaa vya michezo

Uje na raba nyeupe/viatu vya michezo na soksi/ stocking za njano Bukta na t-shirt rangi ya bluu

**NB. Wazazi ambao upatikanaji wa sare za shule utakuwa mgumu wawasiliane na uongozi wa shule kwa msaada zaidi.**

### 2.2 MICHANGO YA SHULE

#### (A) MCHANGANUO WA MICHANGO YA SHULE

| Na. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | Tsh. 65,000/= |
| 2. | Nembo ya shule | Tsh. 5,000/= |
| 3. | Tahadhari | Tsh. 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | Tsh. 5,000/= |
| | **JUMLA** | **Tsh. 80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **BWONGERA SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT: Ac. No. 32701200050 NMB.** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

***(b) Bima ya Afya.***

Jukumu la matibabu ni la mzazi, hivyo mzazi/mlezi anashauriwa kumlipia mtoto wake bima ya afya yaTaifa (NHIF) ambapo shule itawaunganisha na ofisi za NHIF mkoa wa Geita kupata bima hizo. ***Kila mwanafunzi ni lazima aje na bima ya afya ya NHIF. Kwa wale wasiokuwa nazo waje na shilingi 50,400/=*** ili wapatiwe bima hizo na ofisi za bima (NHIF) ya mkoa wa Geita. Malipo hayo ya bima ni kwa mwaka.

(**c.) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni: -**

- Rim moja ya karatasi A4 (Double A)
- Spring file moja kwa ajili ya kutunzia taarifa za maendeleo ya mwanafunzi.
- Daftari za kutosha kwa ajili ya masomo yote zisizopungua 11(counter book)
- Ndoo kubwa (1) moja kwa ajili ya matumizi ya kila siku
- Ndoo moja (lita 10) kwa ajili ya chakula
- Vyombo vya kulia chakula ikiwa ni pamoja na: -Sahani, bakuli,kikombe na kijiko.
- Jembe lenye mpini, reki, fyekeo na panga.
- Fagio la plastic (soft bloom) na fagio la kusukumia maji (hard bloom)
- Njoo na  nakala za vyeti vya kitaaluma pamoja na kuzaliwa
- Godoro jipya futi mbili na nusu.
- Chandarua kimoja kwa ajili ya kujikinga na mbu cha bluu.
- Shuka mbili za rangi ya pinki na bluu kwa ajili ya kutandika na kujifunika.
- Kalamu za kutosha na mathematical set
- **Scientific Calculator fx-991 ms plus.**
- Hati maalumu ya vipimo vya daktari kuthibitisha hali ya Afya yako (fomu imeambatishwa)

3. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya WAZIRI MKUU – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU: KAMWE;**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**NB: Kwa kuwa mwanafunzi harusiwi kumiliki line/simu, shule itaweka utaratibu kwa wazazi/walezi kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu.**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, kuoa au kuolewa, na mahusiano ya jinsi moja.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kusababisha mimba.
xiii. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za inchi.
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali za umma makusudi.

**NB; mzazi au mlezi kama mwanao anachangamoto ya nidhamu nivyema ukaujulisha uongozi wa shule mapema ili wamtambue na kumsaidia.**

4. viambatisho na fomu muhimu.

- FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA [MEDICAL examination form; ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni, kulipa ada za shule, michango na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.
- Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi watakaoweza kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni pamoja na namba zao za simu.

Unatakiwa kutii sheria, taratibu na kanuni zote za shule muda wote uwapo shuleni.
Kutokujua sheria za shule haitakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua.
Kwa kipindi chote utakachokuwa mwanafunzi wa shule hii; utakuwa mwakilishi na balozi mwaminifu wa shule mahali popote utakapo kuwa. Hivyo basi utovu wa nidhamu utakaofanya bila ya kujali mahali au wakati,uongozi wa shule utakuchukulia hatua za kinidhamu zinazostahili dhidi yako.

HEAD OF SCHOOL
BWONGERA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 137,
CHATO.

NOVATI M. UNDERSON
MKUU WA SHULE.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA CHATO**

**Namba za simu**
Mkuu wa shule ***0719801205***

Makamu Mkuu wa Shule ***0749734508***

SHULE YA SEKONDARI BWONGERA,
S.L.P1 37,
CHATO - GEITA

## MAELEZO BINAFSI YAMWANAFUNZI

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi:

1. Jina kamili lamwanafunzi……………………………………………………..…
2. (a) Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………….……
   (b) Kijiji/Mtaa alipozaliwa……………………………………………………..
3. (a) Dini………………………………………………………………………….…
   (b) Dhehebu………………………………………………………………………
4. (a) Ni raia wa Tanzania? (Jibu NDIYO au HAPANA) …………………………………………
   (b) Kama siyo Mtanzania, taja uraia wako na ulete cheti cha uraia……………………………
5. (a)Darasa ulilomaliza…………………………………………………………………
   (b) Shule ulikotoka………………………………………………………………..…
6. (a) Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi…………………………………………………………
   (b) Anwaniya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………..…
   (c) Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi……………………………………………….
7. Mahali unapoishi………………………………………………………….…
8. (a) Unaishi na nani? Taja jina lake kamili……………………………………………….…
   (b) Una uhusiano gani na huyo uliyemtaja?...........................................................
9. Mzazi/Mlezi anafanya kazi gani?..........................................................................
10. Je una ndugu Chato? (Jibu NDIYO au HAPANA). Kama ndiyo, anaitwa nani?.................................................uhusiano …………………………………

    Anaishi wapi………………………….

    Namba yake ya simu………………………………..………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA CHATO**

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0719801205***

Makamu Mkuu wa Shule ***0749734508***

SHULE YA SEKONDARI BWONGERA,
S.L.P 317,
CHATO - GEITA

## FOMU YA KUKUBALI

| |
|---|
| |
| **PICHA YA MWANAFUNZI** |
| |

**A: MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………….. ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Bwongera, nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha ……………

Katika Shule ya Sekondari Bwongera. Naahidi kuwa, nitatii na kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za shule.

…………………………… …………………………

Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

| |
|---|
| |
| **PICHA YA MZAZI/MLEZI** |
| |

**B: MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………………………. Mzazi/Mlezi wa………………………………

Nimeyasoma masharti yote ya mwanangu kujiunga na Shule ya Sekondari Bwongera.

Ninakubali na kuahidi kuwa mwanangu atafuata na kutii masharti yote ya shule. Aidha naahidi nitawajibika kwa kumlipia ada ya shule mwanangu pamoja na michango

mbalimbali ya shule na nitakuwa tayari kushirikiana na shule pindi nitakapotakiwa kufanya hivyo.

| | |
|---|---|
| ............................... | ............................... |
| Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe |

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA CHATO**

**Namba za simu**

Mkuu wa shule ***0719801205***

Makamu Mkuu wa Shule ***0749734508***

SHULE YA

SEKONDARI BWONGERA,

SLP 137

**CHATO-GEITA**

## KIAMBATANISHO B
## MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by a medical office)

Student name ……………………………………………………………………………………
Age ……………………………………………………………………………………………

Blood examination: Hemoglobin
…………………………………………………………………. Any abnormalities Notes
………………………………………………………………………… Stool examination
……………………………………………………………………………………..

Urinalysis ………………………………………………………………………………………

T.B Test (If negative Immunizations given) ……………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

Eyes ……………………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………………………

Any chronic complaints not noted above e.g.

Asthma ………………………………………………………………………………………….
Headache
…………………………………………………………………………………………..

Skin disease etc
……………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

Also anything else that the school staff should know About
………………………………………………………………………………………….

Any treatment given or recommended

……………………………………………………………………

In case of Bilharzias it's recommended that student should attend the Bilharzias clinic before they come to school

………………………………………………………………………………………………..

I certify that I have examined the above student and recommended that she/he fit unfit to pursue Secondary education.

Signature of examiner………………..
Designation ………………………….

Official stamp ……………………
Date ……………………………